


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TAARIFA KWA UMMA

Tarehe: 25/10/2021

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imepokea Tshs. **3,348,225,807.18** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango za mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya **UVIKO 19**, uliozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassani Oktaoba 10, 2021 ambapo triloni **1.3** zilitolewa na kunufaisha wana nchi wa nchi nzima.

Katika mgawo wa Tshs. **3,348,225,807.18** . Uliotolewa kwa Manispaa ya Kinondoni, Tshs. **2,920,000,000/=** zitatumika kujenga Madarasa **146** katika Shule za Sekondari, Tshs. **300,000,000/=** zitatumika kujenga huduma ya dharura Hospitali ya Wilaya Mabwepande, Tshs. **55,417,139.58** zitatumika kujenga miundombinu ya Elimu ya Msingi (vyoo na visima vya maji) na Tshs. **72,808,667.60** zitatumika katika kampeni ya chanjo ya **UVIKO 19**.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mh. Songoro Mnyonge, kwa niaba ya Kamati ya fedha na uongozi na baraza la Madiwani amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassani kwa mgao huo uliowezesha kutatua changamoto mbalimbali katika Manispaa ya Kinondoni., katika Sekta ya Elimu na Afya. Aidha, ameahidi usimamizi mzuri wa fedha hizo ili ziweze kuleta tija.

Imetolewa na

Sebastan M. Mhowera
AFISA UHUSIANO
MANISPAA YA KINONDONI